compass
The Salvation Army's Global Strategic Framework

# Mazungumzo ya Compass
## Maelezo ya Mwezeshaji



Mwongozo wa kukusaidia unapopanga, unapoongoza na kukamata majibu kutoka kwa *Mazungumzo ya Compass* katika eneo lenu.

Karibu kwenye *Mazungumzo ya Compass*! Asante kwa kuwa radhi kuwezesha mazungumzo ya Compass. Tunatarajia utaona maelezo haya yana msaada unapoongoza timu yako katika mazungumzo.

*Mazungumzo ya Compass* ni maswali yaliyo wazi yaliyotengenezwa kusaidia kikao, ushirika au dhihirisho jingine lolote la huduma linalojihusisha na Mfumo wa kazi wa Mkakati wa Jeshi la Wokovu duniani (The Salvation Army's Global Strategic Framework).



**Kwa ajili ya habari zaidi kuhusu Mfumo wa Kazi wa Mkakati Duniani (Global Strategic Framework), tembelea** sar.my/strategy

Mwongozo huu wa Mwezeshaji umetengenezwa ili kukusaidia unapoongoza mazungumzo haya. Hautoi maelekezo bali unatoa mapendekezo ya namna gani uongoze mazungumzo ili uhakikishe yanaendana na hali ya kikao au eneo lako. (Zingatia: 'kikao' kinatumika katika maandishi haya yote ili kuzungumzia huduma yote ya Jeshi la Wokovu katika eneo.)

*Mazungumzo ya Compass* siyo uhakiki rasmi, wala hayajatengenezwa kuchukua nafasi ya mkakati wako binafsi au tathmini ya kikao. Yametolewa kama msaada ili kuhamasisha kutafakari na kukuza hatua za utendaji ambazo nyie wenyewe mtaamua. Yamekusudiwa kutumika katika ngazi ya mahali mlipo – ili kusaidia kikao au dhihirisho jingine la huduma.

Utaona kwamba maswali ni ya shirika na ya kibinafsi kwa wakati mmoja. Mabadiliko siku zote huanza na mtu. *Mazungumzo ya Compass* yanamuuliza kila mtu ajiulize swali yeye mwenyewe – kisha kuliuliza kundi lilitumie swali hilo katika kikao chao.

Vile vile utaona kwamba maswali zaidi ni ya wazi. Yamekusudiwa kuhamasisha majadiliano na mazungumzo zaidi. Uwe huru kuacha hili lifanyike – ni ndani ya mazungumzo yaliyorefushwa, watu wanapojihusisha binafsi na mada, ndipo mafunuo muhimu yatagundulika.


Unakaribishwa sana kuunda maswali ya kwako mwenyewe – mada zinazoendana na wewe na kikao chako. Fikiria kuhusu mada zinazohusu dhana yako – na zizungumziwe.



# Mwongozo wa kuongoza mazungumzo ya kikundi

Hapa kuna kanuni za kuongoza mazungumzo yanayoongozwa. Unaweza kuziona zinasaidia unapojiandaa:

- Ukubwa wa kikundi: Ili kuhamasisha mazungumzo na kuhakikisha kwamba kila mmoja anastarehe, inapendekezwa kwamba mazungumzo haya yaendeshwe katika kikundi kisichozidi watu 10. Unaweza kutumia vikundi kadhaa kama unataka watu wengi wahusishwe.
- Fafanua kusudi na malengo: Unapoanza, elezea wazi kusudi na malengo ya mkutano. Unataka kupata nini kwa ajili ya kikao chako? Unatumaini kukamilisha nini?
- Anzisha sheria za msingi: Weka matarajio ya ushirika wa heshima, usikilizaji makini, na mrejesho wa kujenga.
- Himiza ushiriki: Kimatendo tafuta ushiriki wa washiriki wote, pamoja na washiriki wa kimya, na tengeneza nafasi salama ya kujieleza kwa mtazamo mpana.
- Uwe wazi kwa mawazo tofauti: Kiri na thamini mawazo mbalimbali, hata kama yanatofautiana na yako.
- Simamia migongano: Himiza yapatikane majibu mbalimbali, lakini kama kutokukubaliana kukijitokeza, kisaidie kikundi kifikie mahali pa kukubaliana.
- Uwe tayari kuelekeza upya: Uwe tayari kuelekeza mazungumzo upya taratibu kama yatakwenda nje ya kusudio au kama mtu mmoja akitawala mazungumzo.
- Ruhusu mda kwa wasio wepesi kuongea: Wafikirie watu ambao siyo wepesi wa kujieleza na kwa makusudi waalike watoe michango yao. Usimlazimishe mtu kuongea kama hayuko tayari kufanya hivyo.
- Anza na maswali ya Mazungumzo ya Compass; lakini ruhusu mazungumzo yaendelee kama kawaida – uone yanakupeleka wapi. Epuka maswali yanayoweza kujibiwa na 'ndiyo' au hapana' tu.
- Tumia maswali zaidi kuchunguza mtazamo wa ndani, kuhimiza ufafanuzi, na kuchochea mazungumzo zaidi (tazama hapo juu).
- Maamuzi: Lisaidie kundi lifikie makubaliano au uelewa wa wazi wa mambo ya msingi ya kuondoka nayo.
- Muhtasari: Jinsi mazungumzo ya kila swali yanavyokamilika, toa muhtasari wa yaliyozungumzwa, ukitoa mawazo muhimu ya kufafanua au ya kuongezea.
- Toa hitimisho: Mwisho wa mkutano, washirikishe hitimisho lolote, uamuzi na mpango wa utekelezaji uliokubaliwa.





# Maswali

Hapa kuna maswali ya kufuatilia yaliyopendekezwa ya kukuongoza katika *Mazungumzo ya Compass*:

## Maisha ya Kiroho

Sehemu hii inahusu maisha yetu yote binafsi ya kiroho – yetu wenyewe na yale ya kikao chetu. Fikiria kuanza mazungumzo kwa uzoefu wao wenyewe – kisha wazungumzie kuhusu kikao chao. Kumbuka kwamba kila mmoja ana uzoefu tofauti. Wengine wanaweza kuwa Wakristo wapya huku wengine wanaweza kuwa wamekuwa waamini kwa muda mrefu.

- Tunamfahamu Yesu vizuri namna gani? Je, maisha yetu ya kiroho yanakua kama kanisa na kama watu binafsi?
- Biblia ina umuhimu gani kwangu? Je, ni kipaumbele kikaoni?
- Tunafanya nini kuwasaidia watu wamfahamu Yesu vizuri zaidi?
- Tunafahamu utakatifu kuwa ni nini?
- Karama zangu za rohoni ni zipi? Nazitumia namna gani kutimiza makusudi ya Mungu?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- Tunakuaje kiroho?
- Washauri wetu wa kiroho ni akina nani? Mfikirie aliyewahi kukusaidia. Tunawezaje kufuata mfano wao?
- Tunafanya nini kuwafanya watu wetu wawe wanafunzi wa Yesu, kuwasaidia watu wakue kiroho?
- Nini kingine tunaweza kufanya ili tukue kiroho – kibinafsi na katika kikao chetu?
- Je, ni namna gani mipango yetu, mahubiri yetu na matendo yetu yanawaelekeza wengine kwake Yesu?
- ‘Utakatifu’ maana yake nini na tunawezaje kuuonyesha kwa matendo?

## Maendeleo ya Kiongozi

Lengo: Kuwaendeleza maafisa na viongozi wa huduma wanaoonyesha utumishi wa kweli, na ambao kiroho wamekomaa, wenye uwezo na waliowezeshwa kwa ajili ya majukumu yao ya sasa na yale yajayo.

Sehemu hii inahusu ‘uongozi wa huduma.’ Hii ni pamoja na maafisa wetu wa kikao, majemadari na yeyote mwenye wajibu wa uongozi kikaoni. Lengo ni kuwasaidia wakue na kuendelea katika majukumu yao, kuwatia moyo, na kuwawezesha viongozi wapya.

- Fikiria kuhusu kiongozi wa kipekee uliyemfahamu – nini kilimfanya awe wa kipekee?
- Tunaweza kufanya nini kuwahimiza watu wengi wachukue wajibu wa uongozi?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- Katika kikao chetu nani anatakiwa kuhimizwa aingie katika wajibu wa huduma? Tunaweza kuwasaidia namna gani wajiandae?
- Tunafanya nini ili kushirikiana na vijana wetu? Tunaweza kufanya nini zaidi?
- Tunaweza kufanya nini kuwasaidia viongozi wetu wa sasa wa huduma?
- Ni mafunzo gani ambayo divisheni au teritori yetu inaweza kutoa ili kuwaendeleza viongozi wa sasa na wa siku zijazo?

## Ustawi wa Afisa

Lengo: Kuanzisha mwelekeo wa jumla kwa ustawi wa afisa, tukizingatia afya ya kimwili, kiakili na kiroho pamoja na kutoa mazingira yanayostahili ya kuishi.

Sehemu hii inawafikiria maafisa wa Jeshi la Wokovu. Lengo ni kuwasaidia na kuwatia moyo katika huduma yao. Fikiria kuhusu afisa wako wa kikao pamoja na maafisa wengine duniani unapofanya kazi kupitia maswali ya *Mazungumzo ya Compass*. Ingawa hili linaweza kuonekana kama swala la 'Makao Makuu ya Teritori', lakini kuna mengi tunayoweza kuyatimiza katika ngazi ya chini. Kama wewe ni afisa wa kikao nawe unaongoza mkutano wa *Mazungumzo ya Compass*, uwe muwazi na mwaminifu katika mazungumzo – washirikishe wengine mawazo yako; lakini vile vile kumbuka hili linawahusu maafisa wote.

- Je, maafisa wetu wanastawi? Tunafanya nini kuwatia moyo na kuwasaidia?
- Kwa kufahamu kwamba maafisa wengi duniani hawapokei riziki kamili na/au wanaishi katika mazingira duni, je, tuna lolote tunaloweza kufanya ili kuwasaidia?
- Tunawezaje kuwahimiza watu wafikirie kuhusu uafisa wa Jeshi la Wokovu?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- 'Ujumla' maana yake nini katika swala hili? Uwe maalum.
- Nini huwasaidia watu 'wastawi'?' (Kwa mfano, kwa maafisa hii inaweza kuwa kupata utoshelevu katika huduma, uhakika wa ustawi wa familia, malezi mazuri ya afya, n.k.)
- Eneo hili vile vile huuliza kuhusu watakaji wa uafisa. Kuna watu kikaoni kwako unafikiri wanaweza kuwa wameitwa kuwa maafisa? Unaweza kuwasaidia namna gani?

## Uanachama

Lengo: Kuanzisha uwazi na usahihi wa kuelezea jinsi watu wanavyokuwa sehemu ya ushirika wa Jeshi la Wokovu.

Uanachama ni sehemu muhimu ya kikao cha Jeshi la Wokovu pamoja na kanisa kwa ujumla. 'Uanachama' na 'kuwa sehemu ya' vinaweza kumaanisha vitu mbalimbali kwa watu mbalimbali. Ujiandae kwa majibu ya aina nyingi kwa maswali ya Compass.

- Maana yake nini kuwa 'sehemu ya' ndani ya Jeshi la Wokovu?
- Unajengaje mahusiano ndani ya kikao/ushirika wetu?
- Tunaweza kufanya nini kuwatia moyo watu waungane na kikao/ushirika wetu?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- Kuwa 'sehemu ya' kuna maana gani?
- Maana yake nini kuwa 'mwanachama' wa Jeshi la Wokovu?
- Tunafanya nini kuwaalika watu wapya kwenye Jeshi? Tunafanya nini kuwafanya wajisikie wamekaribishwa na wajisikie kustarehe?
- Tunafanya nini kinachowafanya watu wajisikie wao ni 'sehemu ya' hapa?
- Vikao vingi vinapitia kupoteza wanachama. Tunafanya nini kuwahimiza watu wabakie?



## Mjumuisho wa Utume

Lengo: Kuanzisha kanuni za kikao na ushirika zitakazo jumuisha utume na kuwezesha ukuaji wa waumini.

Maswali haya yanakabiliana na mpangaji wa siku nyingi wa Jeshi la Wokovu: huduma jumuishi. Kujumuisha huduma ya kiroho na kijamii siku zote imekuwa ndiyo tofauti muhimu ya mipango ya Jeshi la Wokovu. Inahusu kujenga mahusiano na jamii yetu ya pale tulipo na kuhakikisha kwamba kila kitu tunachokifanya kinaelekeza kwake Yesu. Njia hii imetengenezwa ili itusaidie tuone jinsi tunavyojumuisha hivi vipaumbele viwili katika kikao chetu.

- Tunafahamu utume wetu vizuri namna gani na tuna wajibu gani ndani yake?
- Tumeungana vizuri namna gani na mipango mingine ya Jeshi la Wokovu iliyo jirani nasi?
- Tunawezaje kuunganisha kikamilifu zaidi familia ya kikao chetu na watu walio katika jamii yetu?
- Nawezaje kuwatumikia watu wengine? Nachangia namna gani kwenye utume na huduma ya Jeshi?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- Ni kwa jinsi gani tunamfanya Yesu ajulikane nje ya kikao chetu?
- Watu wanaotutembelea kikaoni kwetu wanajuaje kwamba sisi ni kanisa? (Hii inaweza kuwa ni kuhusu alama, salamu, na zaidi.)
- Mipango ya Jeshi la Wokovu imeungana vizuri namna gani katika eneo/divisheni yetu (kwa mfano: kikao, shule, duka la hisani, kituo cha makazi, mipango ya afya, n.k.)?

## Agano

Lengo: Kuhakiki Agano la Askari na lile la Afisa ili kuthibitisha kufaa kwake katika Jeshi la Wokovu la karne ya 21.

Neno ‘agano’ kwa ujumla linarejelea ‘makubaliano.’ Katika Biblia na katika kanisa, mara nyingi hutumika kwa kuunganisha na Mungu. Linaweza kutumika kwa ‘makubaliano’ mengine yenye maana ya kiroho. Maswali haya yanaweka kuhamasisha majibu mengi mbalimbali. Ingawa lengo lililoelezwa la mstari huu wa maswali ni kuhusu maagano ya uanachama wa Jeshi la Wokovu – Agano la Afisa, Agano la Askari na Agano la rafiki – unaweza kuona inasababisha majadiliano ya kina kuhusu kikao chako. Kama mwanzo, acha mazungumzo yenyewe yaongoze majadiliano.

- ‘Agano’ maana yake nini?
- Jukumu la Maagano ya Askari na Rafiki ni lipi?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- ‘Agano’ lina maana gani katika dunia ya leo?
- ‘Agano’ lina maanisha nini kwangu mimi?
- Maagano siyo tu yanawahusu maafisa, askari na marafiki. Ni aina zipi nyingine za maagano tunayoyafanya na Mungu? Tunatambuaje haya?

## Mgawanyo wa Rasilimali

'Ufanisi wa Utume' unaelezwa kuwa ni kiwango ambacho mpango au sera huimarisha utume wa Jeshi la Wokovu. Hutusaidia vizuri namna gani tuhubiri habari njema ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji ya wanadamu katika jina lake?

Maswali haya yanazungumzia 'ufanisi wa utume' – namna gani tunawatumia watenda kazi wetu, mali na misaada ya fedha ili kukamilisha utume wa Jeshi la Wokovu. Vile vile inahusu mipango yetu – ili kuhakikisha kwamba kile tunachokifanya, na kile ambacho tungeweza kufanya, vinazingatia vipaumbele vyetu vya kweli – kuhubiri injili ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji ya wanadamu. Sehemu hii inaweza – na lazima – isababishe tutazame mipango yetu kwa undani zaidi. Ingawa siyo uhakiki rasmi, inaweza kutumika tutazame kwa uaminifu yale tunayoyafanya, jinsi gani tunatumia muda wetu, na fedha zetu, na haswa ni kipi kilicho cha muhimu kwetu. Inaweza ikawa ni muda wa kufikiria kutembelea upya mipango yetu ya kukabiliana na mahitaji ya jamii katika dunia ya leo.

- Tunafanya nini sasa ambacho kitakuwa na matokeo ya muda mrefu?
- Je, kuna mipango au shughuli ambazo tumezing'ang'ania, lakini hazitumikii tena kusudi?
- Je, tunawekeza rasilimali zetu (watu, fedha, muda, nafasi) kwa usahihi?

Maswali ya ufuatiliaji yanayowezekana:

- Tunaweza kufanya nini sasa ili kuhakikisha uendelevu na utulivu wa muda mrefu wa kikao chetu?
- Tunafanya nini vizuri sana kinachosambaza habari njema ya Injili?
- Tunafanya kipi vizuri zaidi kinachotusaidia sisi kukabiliana na mahitaji ya majirani zetu?
- Je, kuna mipango ambayo ina ufanisi mdogo? Je, ni wakati wa kuifikiria?
- Ni kiasi gani cha rasilimali zetu tunachokitenga kwa ajili ya mipango ambayo ina ufanisi mdogo katika kuwashirikisha wengine injili au kukabiliana na mahitaji ya watu?
- Kama tukigawa upya rasilimali zetu (watenda kazi, fedha, nafasi), tunaweza kufanya nini badala yake? Tunaweza kutumiaje rasilimali zetu vizuri?

## Maswali machache ya mwisho:

*Wakati wa mazungumzo haya, Mungu amesema nini na wewe?*
*Mungu amekupa utambuzi au mwongozo gani?*
*Utachukua hatua gani kuhusu yale ambayo Mungu anasema?*